HISTORIA YA MAKONGO JUU

1. Mkusanyiko wa mwanzo

Mwaka 1984, Baba Mtakatifu Yohane Paulo II, aliutangaza kuwa Mwaka wa Bikira Maria Mama wa Mungu. Familia ya Mungu duniani kote ilialikwa kumuenzi Mama wa Bwana Wetu kwa kusali Rozari Takatifu katika familia na katika vikundi mbalimbali vya sala.

Hapa Tanzania, Baraza la Maaskofu Katoliki (TEC) lilitoa mwito wa kufanyika mafundisho mbalimbali kuhusu nafasi ya Bikira Maria katika Kanisa na hasa mafundisho ya dogma kuwa Maria ni Mama wa Mungu, huku wanakwaya wakitakiwa kutunga nyimbo mbalimbali za kumuenzi Mama wa Mungu.

Mwaka huo ulikuta eneo la makazi la Makongo Juu likiwa na idadi ndogo ya waamini Wakatoliki huku wakiwa hawana mfumo wowote rasmi wa kuwa pamoja. Baraka za Bikira Maria ziliingia na kupanda mbegu za kudumu kwa familia ya Mungu.

Waamini waliokuwa wanaishi eneo la Makongo Juu na viunga vyake walijikusanya na kuanza kusali Rozari Takatifu katika Kanisa la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hapo, watu wawili, Benedict Momba, wakati huo akiwa ni Katekista wa Chuo Kikuucha Dar es Salaam akiishi Makongo Juu na Evans Nsengimana walikusanya baadhi ya waamini wa Makongo Juu na kuwahamasisha kusali Rozari katika familia zao na baadaye kuunda kikundi kilichokuwa kikikutana mara mbili kwa juma kwa ajili ya kusali pamoja.

Mwaka huo huo kikundi hicho cha waamini 11 kilipata sura na kuwa na uongozi kama ifuatavyo:

1. Teresia Kunundu	Mwenyekiti
2. Severine Lyaruu	M/Mwenyekiti
3. Peter Chea	Mwana Rozari
4. Ester Aloyce	Mwana Rozari
5. Rozaria Nyoka	Mwana Rozari
6. Veronika Nashomba	Mwana Rozari
7. Peter Mboni	Mwana Rozari
8. Fidelis Samweli	Mwana Rozari
9. Katekista Benedict Momba	Mwana Rozari
10. Evans Nsengimana	Mwana Rozari
11. Amandus Yohana	Mwana Rozari

Kikundi hiki kulikuwa kikikutana kila Jumapili na Jumatano alasiri na kusali Rozari katika majengo ya Shule ya Msingi Makongo.

2. Nyumba ya Ibada

Kikundi cha Wanarozari kilikuwa kimeiomba serikali ruhusa ya kutumia majengo ya Shule ya Msingi kwa ajili ya ibada. Pamoja na kukiruhusu kikundi hicho kutumia majengo ya shule kwa ibada zao, Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Serikali aliazimia kuangalia uwezekano wa kukipatia kikundi hiki ardhi ambapo kingeweza kujenga nyumba ya ibada. Wakati huo CCM ilikuwa imeshika hatamu na ikifanya kazi sambamba na Serikali katika utawala.

Ilipofika Oktoba 6, 1984, CCM tawi la Makongo Changanyikeni kilikipa bure kikundi hicho kiwanja chenye ukubwa wa takriban nusu eka kwa ajili ya kujenga nyumba ya ibada. Hapo kukawa na mahali maalum kwa ajili ya kumfanyia Mungu ibada ambapo familia ndogo ya Mungu ikaanza kukutana.

(kiwanja hiki kilikuwa wapi? Kiko wapi hivi sasa? Je, nyumba hiyo ibada ilijengwa?)

3. Misa Takatifu ya kwanza na kuzaliwa kwa kigango

Kikundi kidogo cha watu 11 kilikuwa kama ile 'mbegu uliyoanguka katika udongo mzuri, ikamea ikazaa...' (Mt: 13:8).

Kadri uhamasishaji ulivyozidi kushika hasi, kikundi hiki cha Wanarozari kiliendelea kukua kwa kupata washiriki zaidi. Familia nyingi zaidi zilijiunga na kikundi hiki hivyo kuleta mwamko mpya na mawazo mapya ya maendeleo kiroho. Baadhi ya mawazo ya kimapinduzi yaliyokuja na wanarozari hawa wapya ilikuwa pamoja na kukutana na kusali Rozari Takatifu kila Jumapili na Jumatano, kuwepo pia utaratibu wa kuwa na Ibada ya Misa Takatifu angalau mara moja kwa mwezi.

Wazo hili liliwavutia wanarozari wengi hivyo Septemba 1985 ujumbe ulitumwa kwa Baba Paroko wa Parokia ya Mt Mikaeli Malaika Mkuu, Kawe kumwomba kuangaliauwezekano wa kuwa na adhimisho la Misa Takatifu walau mara moja kwa mwezi hapo Makongo Juu.

Baba Paroko alisita kwanza kwa sababu hakuwa na uhakika kama pangalikuwa na idadi ya kutosha ya waamini kuhalalisha uwepo wa Ibada ya Misa kila mwezi.Baada ya kuhakikishiwa uwepo wa waamini wa kutosha, Baba Paroko Padre Appolinary Kawishe wa Shirika la Mitume wa Yesu aliadhimisha Misa Takatifu kwa mara ya kwanza hapa Makongo tarehe Oktoba 3 1985. Kuanzia siku hiyo Makongo Juu ilitambuliwa rasmi kama Kigango cha Parokia ya Kawe.

Kutokana na idadi ya waamini kuendelea kuongezeka, mahitaji ya kiroho pia yaliongezeka. Ilipofika 1988 iliamuliwa kwamba kuwe na ibada ya Misa Takatifu kila Dominika badala ya mara moja kwa mwezi. Uamuzi huu pamoja na kuwafurahisha Mapadre, uliwatwisha mzigo mzito zaidi kwa kuwa walikuwa wachache na pili walikuwa hawana usafiri wa uhakika. Hivyo, kwa kushirikiana na waamini waliokuwa

wanajitolea, ilibidi zibuniwe mbinu za kuweza kuhakikisha Ibada ya Misa Takatifu inapatikana kweli kila Dominika.

Uongozi Hairakia wa Parokia ya Kawe na ule wa Chuo Kikuu ulikubaliana kuwa Mapadre wa Chuo Kikuu watakuwa wanaadhimisha Misa Takatifu Makongo Juu kila siku ya Dominika saa 4:00 asubuhi isipokuwa Dominika ya kwanza ya kila mwezi ambapo Mapadre wa Kawe wangeadhimisha Misa hiyo. Utaratibu huu wa Mapadre wa Kawe kuwa wanakuja angalau mara moja kwa mwezi ulilenga kuhakikisha kwamba waamini wa Makongo Juu wanaendelea kuwa na uhusiano wa karibu na Parokia ya Kawe kwa kuwa Makongo Juu ni sehemu ya utawala wa Paroko wa Kawe.

Waamini wa Makongo Juu kwa upande wao walipewa jukumu la kuhakikisha Mapadre wa Chuo Kikuu wanapata usafiri kila wanapotakiwa kuja kutoa huduma hapo kigangoni.

Pamoja na kuwa na utaratibu huu mahsusi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kigango pia kilikuwa kikipata huduma kutoka kwa Mapadre wanaofanya kazi katika Sekretarieti ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) Kurasini, Kituo cha Bethania kilichopo Upanga, na Nyumba Mama ya Wamisionari wa Afrika (Atiman House)iliyopo jirani na Kanisa Kuu la Mt. Yosef wakati ambapo Mapadre kutoka Chuo Kikuu walipokosekana.

Mapadre wa Chuo Kikuu waliokuwa wakihudumia walikuwa ni Prof. Padre Daniel Mkude na Prof. Padre Cosmas Mogella kwa upande wa TEC alikuwa Padre Method Kilaini, ambaye baadaye alikuja kuwa Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam na Padre Paul Haule, kutoka Nyumba Mama ya Wamisionari wa Afrika (Atiman House) alikuwa ni Padre Wolfgang na kutoka Bethania House alikuwa Padre Canute Mlowe.

Mapadre hawa walihakikisha kuwa haitokei hata Dominika moja ambapo kondoo wa Bwana Makongo Juu wanabaki bila mchungaji.

4. Ununuzi wa eneo la kanisa

Maandalizi ya ujio wa Kigango na hatimaye kuwa Parokia yalihitaji kuwa na mahali maalum, hivyo ulianza mkakati wa kutafuta eneo lifaalo kwa ajili ya kujenga Kanisa, nyumba ya Mapadre pamoja na majengo mengine.

Julai 10, 1988 waamini wa Makongo Juu walinunua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa kanisa kiasi cha hekta kama mbili hivi kutoka kwa muamini mmoja, Mzee Yohana Ngoya Mwanalongo kwa kiasi cha Sh. 300,000 zilizolipwa kwa awamu tatu. Muamini huyo pia alitoa bure ardhi ya ukubwa wa kama nusu ekari kwa ajili makaburi ya Wakatoliki.

5. Ujenzi wa Ukumbi

Tangu kuanzishwa kwa Kigango hadi kuwa Parokia, waamini wamekuwa wakitumia ukumbi kwa ajili ya ibada, na kwa muda mrefu imejulikana kama ndio Kanisa la Makongo Juu.

Ujenzi wa jengo hili ulianza Septemba 13, 1989 ukitarajiwa kuwa ukumbi wa shughuli mbalimbali (*Multipurpose Hall).*Awamu ya kwanza ya ujenzi wa ukumbi wa shughuli mbalimbalikatika kiwanja kilichonunuliwa mwaka 1988 ulianza chini ya usimamizi wa Edward Mhagama. Ujenzi huu licha ya kuwa ulikuwa inaendelea kwa kasi ndogo sana na kwamba jengo lenyewe lilikuwa linajengwa katikati kabisa ya kiwanja, kinyume na maelekezo ya uongozi wa Kigango, ulikumbwa na matatizo mengi ya kiufundi, hivyo ukasitishwa na Halmashauri.

Septemba 28, 1991, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mhashamu Polycarp Pengo, kwa mara ya kwanza alitembelea Kigango cha Makongo na kuadhimisha Misa Takatifu katika viwanja vya shule ya Msingi Makongo.

Katika ibada hiyo, wakatekumeni wanane walibatizwa, 21 walipata Sakramenti ya Kipaimara na watatu walibariki ndoa zao. Hawa walikuwa malimbuko ya kusanyiko la Mungu Makongo Juu.

Akijibu risala ya waamini wa Makongo Juu, Mhashamu Askofu Pengo aliwapongeza waamini kwa kupata ardhi kwa ajili ya kujenga nyumba ya Mungu. Akiwahimiza kuharakisha ujenzi wa Kanisa ili waweze kuondokana na adha ya kuendelea kutumia majengo ya Shule ya Msingi ya kwa ibada.

Tarehe 21 Septemba 1992, awamu ya pili ya ujenzi wa ukumbi ulianza chini ya usimamizi wa Kamati yenye wajumbe wafuatao:

1.	Benedict Mwobahe	Mwenyekiti
2.	L.M. Kiswaga	Mjumbe
3.	Severine Lyaruu	Mjumbe
4.	Simon Billa	Katibu

Kamati hii ilipewa hadidu za rejea zifuatazo:

(a) Ukumbi huo ujengwe pembeni kabisa mwa kiwanja ili kutoa nafasi ya ujenzi wa kanisa, nyumba ya mapadre, nyumba ya masista, shule ya awali na zahanati hapo baadaye.
(b) Ujenzi uzingatie kwamba jengo hilo litatumika kama kanisa kwa muda mrefu hivyo liwe na Altare na Sakristia.

Agosti 20 1994, ujenzi wa ukumbi ulikamilika na kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Padre Juvenarius Muba wakati huo akiwa ni 'Vicar General' wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Siku hiyo ndiyo siku ambayo Misa Takatifu iliadhimishwa katika jengo hilo

kwa mara ya kwanza. Sakramenti ya ubatizo, Komunio ya Kwanza na Kipaimara zilitolewa.

Februari 18, 1995 Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu wa Jimbo alikuja kuadhimisha Misa Takatifu hapo Makongo Juu. Madhumuni ya ziara hiyo ilikuwa kuja kujionea hatua ambayo waamini walikuwa wamefikia katika kukiendeleza kiwanja cha Kanisa.

Agosti 30, 1997, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo alikuja kutoa Sakramenti ya Kipaimara hapa kigangoni Makongo Juu. Pamoja na kazi hii ya kiuchungaji, Mwadhama alitoa agizo kuwa ni vizuri Kigango kikajiwekea mkakati wa kukiandaa kuwa Parokia ifikapo mwaka 2002.

Septemba 24, 1998, mpango wa matumizi ya ardhi (master plan) wa Kigango ambao ulijumuisha ujenzi wa kanisa, nyumba ya mapadre, nyumba ya masista, shule ya awali, zahanati, pamoja na michoro sanifu ya nyumba ya mapadre na shule ya awali uliidhinishwa rasmi na Mwadhama Kardinali Pengo.

Juni mosi, 1999, mpango wa maendeleo ya kiroho na kimwili wa miaka miatu 1999/2002 wa kigango cha Makongo Juu ulizinduliwa rasmi na kuanza kutekelezwa. Dhamira kuu ya mpango huo ilikuwa kukiandaa Kigango kuwa Parokia ifikapo 2002 na ulikuwa na sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ilianisha miundombinu ambayo ilitakiwa kuwapo kabla ya kigango kuwa Parokia na mikakati ya namba ya kujenga miundo mbinu hiyo. Sehemu ya pili ilianisha shughuli za kiroho ambazo zilitakiwa kufanywa ili kuwandaa waamini kiroho, kifikra na kisaikolojia ili wamudu kubeba majukumu ya kuwa Parokia.

5. Ujenzi wa nyumba ya Mapadre

Katika kujiandaa kuwa Kigango na kupata wachungaji watakaoweza kuishi kati yetu, ilionekana kuwa ni lazima kuwepo na makazi rasmi ya Mapadre ambapo Agosti 1999, ujenzi wa nyumba ya Mapadre ulianza chini chini ya Kamati ya Ujenzi ikiongozwa na Evaristo Liwa kama Mwenyekiti na E. Mhango (sasa marehemu) na Severine Lyaruu kama wajumbe. Kamati hii baadaye iliongozwa na Rogart Kisanga. Baada ya Kisanga kwenda Swaziland, Deo Mugishagwe aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa kamati hiyo.

Novemba 14, 1999, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo aliweka jiwe la msingi ka nyumba hiyo ya Mapadre na akapanda mti wa WAWATA na Mti wa Milenia mahali ambapo pango la Mama Bikira Maria litajegwa.

Baada ya nyumba ya Mapadre kukamilika, mnamo tarehe 2 Machi 2005, Askofu Mkuu wa Dar es Salaam, Mwadhama Policarp Kardinali Pengo alimtuma Padre Martin Dominic kuwa Padre Mkazi katika Kigango cha Makongo Juu.

Kikao cha dharura cha Halmashauri ya Walei Kigango cha Makongo kiliitishwa mahsusi kutoa fursa kwa wajumbe wa Halmashauri kukutana rasmi na Padre Mkazi.

Moja ya maazimio ya kihistoria yaliyofanywa na Halmashauri katika kikao hicho ilihusu umuhimu wa kuweka katika maandishi historia Kigango. Kazi ya kuandika historia hiyo ilipewa kipaumbele cha hali ya juu, na hivyo ilipofika Agosti 2005 toleo la kwanza la historia ya Kigango chetu kwa kipindi cha 1984 hadi 2004 lilitokana na kuzinduliwa rasmi katika katika ibada ya Misa Takatifu siku ya Sikukuu ya Somo wa Kigango Oktoba 7, 2006.

6. Kuzaliwa Parokia

Julai 7, 2017 ndio siku ambayo kikundi kidigo cha wanarozari waliokuwa wakikutana mara mbili tu kwa juma, kilikua hadi kufikia kuwa Parokia ya Bikira Maria Mama wa Rozari Takatifu. Tangazo lililotolewa na Askofu Mkuu wa Dar es Salaam, Mwahdama Policarp Kardinali Pengo, pamoja na kutangaza Parokia, pia lilimteua Padre Mkazi wa Makongo Juu Mheshimiwa Martin Dominic kuwa Parokia wa Parokia ya Mlandizi na Padre Maximilian Wambura aliyekuwa Paroko Msaidizi wa Parokia ya Familia Takatifu Mburahati kuwa Paroko wa kwanza wa Makongo Juu.

Wachungaji waliochunga kundi Makongo Juu kama Maparoko kartka kipindi hicho ni

1. Maximillian Wambura (2007 – 2012)
2. Gallen Mvungi (2012 – 2014)
3. Joseph Massenge (2014 –

Pamoja nao, kwa vipindi mbalimbali, mapadre wengi wamepitia katika Parokia ya Makongo Juu, wengi wao wakiwa wanasoma ama Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au Chuo Kikuu cha Ardhi. Hao ni pamoja Padre Eusebius Nzigilwa, aliyekuwa akisoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Padre Andrea Dimosso kutoka Jimbo la Morogoro aliyekuwa akisoma Chuo Kikuu cha Ardhi

7. Ujenzi wa Kanisa

Ndoto ya kuwa na Parokia yenye miundombinu inayotosheleza mahitaji ilianza kuonekana kuwa kweli mapema sana. Tayari kulikuwa na ukumbi uliokuwa ukitumika kama kanisa, na nyumba ya Mapadre. Jengo moja muhimu lilikuwa bado – nalo ni kanisa.

Februari 2, 2000 Halmashauri ya Kigango alimuomba rasmi Camilus Lekule, msanifu wa majengo wa Afri-Arch Associates, asanifu kanisa ambalo lingejengwa hapo baadaye. Hadidu za rejea alozopewa ni kama ifuatavyo:

i. Kanisa liweze kuchukua watu kati ya 800-1000

ii. Kanisa lisanifiwe kwa namna ambayo upanuzi wa baadae uwezekane pindi panapokuwa na haja ya kufanya hivyo.
iii. Liwe nadhifu kuwiana na unadhifu wa nyumba ya Mapadre iliyokuwa inajengwa.

Michoro ya awali ya modeli ya kanisa hilo iliwasilishwa na Dr Lekule kwenye kikao cha pamoja na Kamati ya Tendaji ya Kigango, Kamati ya Ujenzi na Kamati ya Michango pamoja na watu mashuhuri wa Kigango, hususan Damian Meela, Silvin Mongella tarehe 20 Januari 2001 na ikaidhinishwa.

Mwaka 1987 ulikuwa ni mwaka wa Uchaguzi wa viongozi wa Halmashauri ya Walei katika Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Kigango cha Makongo Juu kilishiriki kwa mara ya kwanza katika uchaguzi huu. Ili kuweza kuchagua viongozi, kigango kiligawanyika katika Kanda tatu kama ifuatavyo.

1. Kanda ya Makongo Chini
2. Kanda ya Makongo Juu
3. Kanda ya Makongo Mbezi/Changanyikeni

Waamini wa kila kanda walichagua viongozi wawili ambao walijulikana kama walezi wa Kanda. Wafuatao walichaguliwa:

1. **Kanda ya Makongo Chini**
   Teophil Nshiku
   David Makene
2. **Kanda ya Makongo Juu**
   Silvin Mongella
   Severin Lyaruu
3. **Kanda ya Makongo Mbezi/Changanyikeni**
   Martin Busanda
   Timothy Kasella

Walezi hawa wa kanda ndiyo waliofanya uchaguzi wa viongozi Agosti 2, 1987 na wafuatao walichaguliwa:

Timothy Kasella	Mwenyekiti
Severin Lyaruu	Makamu Mwenyekiti
D. Mizambwa	Katibu

Ilipofika Mei 1991, Kigango kilianzisha mfumo wa Jumuiya Ndogondogo za Kikristo, Jumuiya sita ziliundwa kama ifuatavyo:

1. Jumuiya ya Mt. Cesilia
2. Jumuiya ya Mt. Theresia wa Mtoto Yesu
3. Jumuiya ya Mt. Thomas
4. Jumuiya ya Mt. Francis
5. Jumuiya ya Mt. Yuda Tadei
6. Jumuiya ya Mt. Agatha

Jumuiya hizi zilizinduliwa rasmi na Mhashamu Askofu Mkuu Polycarp Pengo tarehe 28 Septemba 1991 alipotembelea Kigango cha Makongo kwa mara ya kwanza. Pamoja na kuunda Jumuiya Ndogondogo za Kikristo mwaka huo pia ulikuwa ni mwaka wa uchaguzi, hivyo tarehe 21 Aprili 1991 wajumbe wa Halmashauri ya Walei Kigango walichaguliwa kama ifuatavyo:

Chris Mwalongo	Mwenyekiti
David Makene	Makamu Mwenyekiti
Swithan Billa	Katibu
Martin Busanda	Mhazina
Benedict Mwombahe	Mjumbe na mwenyekiti wa Littrujia
Silvin Mongella	Mjumbe
Ritha Mbotto	Mjumbe
L. Kiswaga	Mjumbe
Severine Lyaruu	Mjumbe

Kufuatia kifo cha Mwenyekiti Chris Mwalongo Aprili mosi, 1994, na kujiuzulu uongozi kwa Makamu Mwenyekiti David Makene kwa sababu ya kujiunga na Wanamaombi, Halmashauri ilimchagua Benedict Mwombahe kukaimu uwenyekiti hadi uchaguzi ulipofanyika.

Ilipofika mwaka 1998, baada ya kuwa na ongezeko kubwa la waamini, Kigango kiligawanywa upya katika mitaa minne, kila Benedict Mwobahe kukaimu uwenyekiti hadi uchaguzi ulipofanyika.

8. Kuzaliwa Parokia

A. MTAA WA MAKONGO MASHARIKI

1. Jumuiya ya Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili
2. Jumuiya ya Mt. Cesilia
3. Jumuiya ya Mt. Michael
4. Jumuiya ya Mt. Gabriel

B. MTAA WA MAKONGO KATI

1. Jumuiya ya Mt. Teresia wa Mtoto wa Yesu
2. Jumuiya ya Mt. Yuda wa Tadei
3. Jumuiya ya Mt. Petro
4. Jumuiya ya Mt. Joseph

C. MTAA WA MAKONGO KASKAZINI

1. Jumuiya ya Mt. Andrea
2. Jumuiya ya Mt. Rafael
3. Jumuiya ya Mt. Augustino
4. Jumuiya ya Mt. Francis

D. MTAA WA MAKONGO MAGHARIBI

1. Jumuiya ya Mt. Paulo
2. Jumuiya ya Mt. Lucia
3. Jumuiya ya Mt. Kalori Lwanga
4. Jumuiya ya Mt. Yohana

Muundo huu ndio uliotumika hadi Februari 18, 2006

MATUKIO MUHIMU KATIKA UHAI WA KIGANGO

4.1 Mwanzoni mwa mwaka 1984, waamini wakazi wa Makongo wapatao 11, baada ya kuhamasishwa wa waamini toka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Evans Nsengimana na Benedict Momba, wakati huo akiwa Katekista wa Chuo Kikuu, walianzisha kikundi cha kusali Rozari kila siku ya Jumatano na Jumapili. Viongozi wa kikundi hicho walikuwa ni:

Theresia Kunundu	Mwenyekiti
Severine Lyaruu	M/Mwenyekiti
Mama D. Mizambwa	Katibu

Octoba 3, 1985 Misa Takatifu iliadhimishwa kwa mara ya kwanza hapo Makongo na Padre Apolinary Kawishe, aliyekuwa Paroko wa Parokia ya Kawe. Padre Apolinary Kawishe alikuja kuadhimisha Misa ya kuombwa na kikundi hicho cha wanarozari.

Agosti 2,1987 uchaguzi wa kwanza wa viongozi wa Halmashauriya Walei ya Kigango ulifanyika baada ya Kigango kugawanywa katika Kanda tatu na viongozi wa Kanda waliojulikana kama Walezi kuchaguliwa kama ifuatavyo:

1. **Kanda ya Makongo chini**
   Teophil Nshiku
   David Makene
2. **Kanda ya Makongo Juu**
   Silvin Mongella
   Severin Lyaruu
3. **Kanda ya Makongo Mbezi/Changanyikeni**
   Timothy Kasella
   Martin Busanda

Julai 1988 Uongozi hairakia wa Parokia ya Kawe ulikubaliana na Mapadre wa Chuo Kikuu kuwa Misa Takatifu itakuwa inaadhimishwa Makongo kila Jumapili na Mapadre wa Chuo Kikuu isipokuwa Jumapili ya kwanza ya kila mwezi ambapo Misa hiyo ingeadhimishwa na Padre kutoka Kawe.

Waamini wa Makongo walipewa jukumu la kutoa usafiri kwa Mapadre wa Chuo Kikuu. (Taz 3.1)

Tarehe moja Juni, 1999, mpango wa maendeleo ya kiroho na kimwili wa miaka miatu 1999/2002 wa kigango cha Makongo Juu ulizinduliwa rasmi na kuanza kutekelezwa. Dhamira kuu ya mpango huo ilikuwa kukiandaa Kigango kuwa Parokia ifikapo 2002 na ulikuwa na sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ilianisha miundombinu ambayo ilitakiwa kuwapo kabla ya kigango kuwa Parokia na mikakati ya namba ya kujenga miundo mbinu hiyo. Sehemu ya pili ilianisha shughuli za kiroho ambazo zilitakiwa kufanywa ili kuwandaa waamini kiroho, kifikra na kisaikolojia ili wamudu kubeba majukumu ya kuwa Parokia.

Mnamo tarehe 2 Februari 2000 Halmashauri ya Kigango ilimuomba rasmi Dkt. Camilus Lekule, msanifu wa majengo wa Afri-Arch Associates, asanifu kanisa ambalo lingejengwa hapo baadaye. Hadidu za rejea alozopewa ni kama ifuatavyo:

i. Kanisa liweze kuchukua watu kati ya 800-1000
ii. Kanisa lisanifiwe kwa namna ambayo upanuzi wa baadae uwezekane pindi panapokuwa na haja ya kufanya hivyo.
iii. Liwe nadhifu kuwiana na unadhifu wa nyumba ya Mapadre iliyokuwa inajengwa.

Michoro ya awali ya modeli ya kanisa hilo iliwasilishwa na Dkt. Lekule kwenye kikao cha pamoja na kamati ya utendaji ya Kigangoni, Kamati ya Ujenzi na Kamati ya Michango pamoja na mashuhuri wa Kigango, hususan Damian Meela, Silvin Mongella tarehe 20 Januari 2001 na ikaidhinishwa.

Tarehe 13 Februari 2000, Askofu Mteule Padre Method Kilaini kwa ombi maalum la waamini wa Kigango cha Makongo Juu, alikuja Kigangoni na kuadhimisha Misa Takatifu ya shukrani, na kumpongeza kwa kuteuliwa kwake kuwa Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam. Waamini walimpa zawadi mbalimbali ikiwa ni pamoja na nguo za Misa. Akajibu risala ya waamini, Askofu mteule Method Kilaini alikiri kuwa tangu uteuzi wake waamini wa Makongo walikuwa wa kwanza kumpongeza, hivyo akaahidi kutowasahau kamwe katika sala zake.

Tarehe 23 Novemba 2000, Msalaba wa Milenia ulipokelewa kwa shangwe na nderemo na waamini wa Kigango na kuzungushwa katika Jumuiya 14 za Kigango. Kila ulipofika msalaba katika Jumuiya, wanajumuiya walisali kituo cha njia ya msalaba.

Mnamo mwezi Machi 2001, Halmashauri ya kigango, kupitia kamati yake ya m iliandaa tamasha la kwaya ili kuchangisha fedha za kununua mabati ya kuezesha nyumba ya Mapadre.

Mgeni rasmi katika tamasha hilo alikuwa Mheshimiwa Askofu Method Kilaini. Kiasi cha Sh. 8,000,000 zilipatikana.

Tarehe 13 Desemba 2002 nyumba ya Mapadre ilikamilika kuezekwa.

Mnamo tarehe mosi Juni, 2003, Halmashauri kupitia kamati yake ya michango iliandaa harambee ili kutafuta fedha za kuwezesha kupiga lipu nyumba ya Mapadre. Mgeni rasmi alikuwa mheshimiwa Yusufu Makamba, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mheshimiwa Padre Pius Rutechura, Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, aliongoza Misa Takatifu siku hiyo. Kiasi cha shilingi milioni 22 zilipatikana Fedha hizi zilitumika kuweka fremu za milango na madirisha, mabomba ya maji na umeme, kupiga lipu ndani na nje kuweka sakafu. Kazi hii ilikamilika Oktoba 25, , 2003.

Tarehe 18 Julai 2004 Mhashamu Askofu Method Kilaini, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam alikuja kigangoni kutoa Sakramenti ya Kipaimara na kuzindua harambee ya kukamilisha ujenzi wa nyumba ya Mapadre. Akazindua harambee hiyo mhashamu alitoa changamoto kwa waamini kuwa ikiwa watafanikiwa kukamilisha angalao wingi moja ya jengo hilo, Baba Askofu angekuja kulala hapa Kigangoni na kusherehekee sikukuu ya Noel kwa kuadhimisha misa ya usiku na mchana. Ahadi hii ilikuwa ni changamoto kubwa katika kukamilisha ujenzi wa nyumba hii.

Tarehe 23 Desemba 2004, ujenzi wa sehemu moja (Wing A) ya nyumba ya Mapadre ilikamilika. Shukrani za pekee zinastahili kutolewa kwa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA) wa Kigango cha Makongo Juu, ambao pamoja na kushiriki katika michango ya kufanikisha ujenzi huu uliokuwa unawakabili waamini wote wa Kigango kwa ujumla, akina mama hawa walijiwekea utaratibu wa kuchangia ununuzi wa vyombo vyote vya ndani ya nyumba hiyo ikiwa ni pamoja na vyombo vya jikoni, vitanda, mapazia, samani, n.k. utaratibu huu ambao waliuita “Mchango wa Kapu la Mama kwa ajili ya Nyumba ya Mapadre” ulikusanya kiasi cha Sh. 1,900.000 na hivyo kuifanya nyumba hiyo iweze kufunguliwa rasmi kwa ibada na Mhashamu Askofu Method Kilaini Desemba 24, 2004. Askofu Kilaini alifuatana na Mheshimiwa Padre Martin Dominic na Frt. Gallen Mvungi na ndiyo walikuwa watu wa kwanza kulala katika nyumba hiyo siku kama alivyoahidi Baba Askofu Julai 18, 2004 (taz. 15.19)

Akiwahutubia waamini wa Kigango cha Makongo Juu wakati wa ibada ya Mkesha wa Noeli, Baba Askofu Kilaini aliwapongeza kwa kazi nzuri waliyofanya ya kukamilisha wingi hiyo kwa kiwango cha hali ya juu kabisa. Hivyo akasema isingalikuwa vema kufunga nyumba hiyo mara atakapoondoka. Kwa hali hiyo aliamua kumwacha Kigangoni Padre Martin Dominic kama Padre Mkazi ili huduma zote za kiroho ziweze

kupatikana hapa hapa. Ili Padre Martin asijisikie mpweke mno, alitangaza pia kuwa Frt. Mvungi atabaki Makongo Juu hadi atakapomaliza kipindi chake cha uchungaji.

Uamuzi huu wa Mhashamu Askofu ulipokelewa kwa shangwe, nderemo na chereko chereko na waamini wa Makongo na kuishia kwa wimbo wa 'Ni Neno Jema Kumshukuru'uliotungwa na Ansbert Ngurumo.

Kufuatia ziara ya kufahamiana iliyofanywa na Padre Mkazi wa Kigango cha Makongo Juu, Mh. Padre Martin Dominic katika mitaa na JNNK za Kigango miezi minne ya kwanza ya ujio wake Januari 2005 – Aprili, umuhimu wa Kigango kuwa na mpango wa maendeleo wa maisha ya kiroho na kimwili wa muda mrefu ambao dira/dhamira ya Kigango ingetamkwa ilidhihirika wazi. Hivyo, Kamati ya watu wanne ya kuandaa mpango huo iliteuliwa na mkutano wa pamoja na Kamati Tendaji na Kamati ya Fedha, Mipango na Uchumi ya Halmashauri kama ifuatavyo:

Timothy Kasella	-	Mwenyekiti
Benedict Mwobhahe	-	Katibu
Padre Martin Dominic	-	Mjumbe
Frateri Gallen Mvungi	-	Mjumbe

Rasimu ya mpango huu wa maendeleo ya maisha ya kiroho na mwili wa miaka kumi (Julai 2005 – Juni 2015) iliidhinishwa na Kamati na Kamati Tendaji na Halmashauri ya Kigango na hatimaye kuzinduliwa rasmi na Mhashamu Method Kilaini tarehe 31 Julai 2005 alipokuja kigangoni kutoa Sakramenti ya Kipaimara. Mpango huu ndio uliokuwa unaongoza shughuli zote za kiroho na kimwili za Kigango na sasa Parokia.

Baada ya muamini kujitolea kununua Tablenakulo kwa gharama ya Sh. 1,000,000 kutoka Peramilo na kujengewa kanisani na Mheshimiwa Bruda Polycarp, umuhimu wa kulikarabati kanisa ili kuimarisha usalama na kuboresha unadhifu wa madhabahu ulidhihirika. Mheshimiwa Padre Martin Dominic, Padre Mkazi alihimiza kwa namna ya pekee ukarabati huo mpaka ikabidi amtoe Yesu Kristo ndani ya Tablenakulo hiyo hadi ukarabati ulipokamilika. Hatua hii iliwashtua na kuwaamsha waamini na hivyo Jumapili za tarehe 5 na 12 Juni 2005 waamini walichanga Sh. 5,566,040 ambazo zilitumika kwa ajili ya kukamilisha kazi za ukarabati zifuatazo:

- Kutengeneza na kuweka madirisha na milango mipya, magrili ya madirisha na milango ya kanisa.
- Kukarabati sakafu ya Kanisa na kuweka marumaru madhabahuni na njia zote kuelekea madhabahuni kutoka milango midogo na mikubwa ya kanisani.
- Kutengeneza Altare na mibali mpya kwa mbao za mninga.

Kazi zote hizi zilikamika Julai 29, 2005 hivyo kumwezesha Padre Mkazi amrejeshe Yesu Kristo ndani ya Tabenakulo tarehe 20 Julai 2005 tayari kwa ujio wa Mhashamu Askofu Method Kilaini tarehe 31 Julai 2005 kuja kutoa Sakramenti ya Kipaimara.

Padre Martin Dominic Rutayebesibwa alipoteuliwa kuwa Padre Mkazi wa Kigango cha Makongo Juu tarehe 24 Desemba 2004, kigango kilikuwa na vyama/vikundi vya kitume sita tu vifuatavyo:

- WAWATA
- VIWATA
- Utoto Mtakatifu
- Ministranti
- Kwaya ya Mtakatifu Bikira Maria Mama wa Rozari Takatifu
- Kwaya ya Mt. Felista

Moja ya mambo yaliyojitokeza wakati wa ziara aliyofanya Padre Mkazi katika kanda na JNNK mwezi Januari hadi Aprili, 2005 ni hitaji la kuamsha miongoni mwa waamini moyo wa ibada kupitia vyama vya kiroho vya kitume. Hivyo hatua za makusudi zilichukuliwa na Padre Mkazi ikiwa ni pamoja na kuwaalika viongozi mbali mbali wa vyama vya kitume ngazi za Jimbo kuja kuhamasisha na matunda ya juhudi hizi yalianza kuonekana mwezi Aprili 2006 kwa kuanzishwa kwa vyama vifuatavyo:

- Neokatekumenato
- Moyo Mtakatifu wa Yesu
- Chama cha Miito
- UWAKATA (Utume wa Wanaume Katoliki)
- Chama cha wasoma Masomo
- VIJANA

Vyama hivi vimesaidia kwa kiasi kuamsha moyo wa ibada na uchaji wa moyo miongoni mwa waamini wa kigangoni.

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa uchaguzi mdogo wa kamati Tendaji unafanyika baada ya kamati iliyokuwa chini ya uenyekiti wa Dkt. Mfungahema kujiuzuru na unakuwa na wigo mpana wa wajumbe, Padre mkazi alichukua fursa hiyo kuzigawa JNNK upya ili kuhakikisha kuwa ukubwa wa jumuiya unakuwa na familia zisizopungua saba na zisizozidi 15. Ili kuhakikisha zoezi hilo linafanyika kwa ufanisi, mnamo tarehe 30 Novemba 2005, Padre mkazi aliteua kamati maalum ya kuratibu ugawanywaji wa jumuiya hizo pamoja na mchakato mzima wa uchaguzi huo mdogo kuanzia JNNK mpya zitakazoanzishwa hadi uchaguzi wa Kamati Tendaji.

Wafuatao waliteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hiyo:

Benedict Mwobahe	-	Mwenyekiti
Mary Ngole	-	Katibu
Timothy Nkondola	-	Mjumbe
Damian Meella	-	Mjumbe
Mtaita	-	Mjumbe
A. Ndibalema	-	Mjumbe
Frateri Denis Wigira	-	Mjumbe

Zoezi hili lilipokamilika, JNNK ziliongezeka kutoka jumuiya 16 na Kanda 4 hadi kufikia jumuiya 32 na Kanda 6. Mgawanyo huu mpya wa Jumuiya hizi si tu ulifanikisha uchaguzi huo mdogo bali pia uliboresha kwa kiasi kikubwa uendeshaji wa jumuiya hizo. Wanajumuiya kwa sababu ya udogo wa Jumuiya hizo waliweza kufahamiana na kushirikiana katika shida na raha.

Mwezi Mei wa kila mwaka ni mwezi wa Mama Bikira Maria. Aprili 30, 2006 jioni saa 11:30 kuliadhimishwa Misa Takatifu ya uzinduzi wa mwezi wa Bikira Maria. Kwa sisi waamini wa Kanisa Katoliki la Makongo Juu, Mama Bikira Maria wa Rozari Takatifu, ni somo na mlinzi wa kanisa letu, hivyo katika ibada hiyo, tulimuenzi kwa namna ya pekee kwa kuwa na matukio ya kihistoria makubwa mawili:

(i) Sanamu kubwa ya Bikira Maria Mama wa Rozari Takatifu juu ya stendi maridadi ya mbao za mninga ilibarikiwa na kusimikwa rasmi kanisani.

(ii) Sanamu ndogo ya Mama Maria pia ilibarikiwa na utaratibu wa kumuenzi mama Mama Maria kwa kuitembeza sanamu hiyo katika Jumuiya zetu, familia hadi familia kwa kipindi chote cha mwezi Mei wa kila mwaka.

Mwezi Oktoba ni mwezi wa Rozari Takatifu. Hivyo, waamini hualikwa kusali rozari katika familia zao, jumuiya hadi ngazi ya Kigango/. Tmnamo tarehe 01 Oktoba 2006, Rozari maalumu ilibarikiwa wakati wa ibada ya misa takatifu, na utaratibu wa kuizungusha rozari hiyo katika jumuiya–zote, kutoka familia moja hadi nyingine ulifanyika kwa kipindi chote cha mwezi Oktoba, 2006 ili kuhamasisha kusali rozari siku zote.

4.2 Kipindi cha kuanzia tarehe 22 Oktoba 2005 hadi 15 Julai 2007, takribani miezi 30, kilishuhudia mabadiliko ya mara kwa mara ya uongozi wa kigango ngazi ya Kamati tendaji ya Halmashauri Walei kwa sababu mbali mbali kama ifuatavyo.

(i) Oktoba 22, 2005 Kamati Tendaji chini ya mwenyekiti wa Dr. R. Mfungahema ilijiuzuru kwa sababu ya kutokuwa na muda wa

kutosha wa kutekeleza majukumu yao katika kanisa kwa sababu ya kuwa na kazi nyingi katika ajira zao.

(ii) Februari 19, 2005 uchaguzi mdogo kujaza nafasi iliyoachwa wazi kufuatia kujiuzuru kwa Dr. Mfungahema na wenzake alifanyika chini ya usimamizi wa mheshimiwa Balozi Nicolaus Kuhanga, Mwenyekiti wa Halmashauriya Walei Jimbo na wafuatao walichaguliwa:

Dkt. Mary Mboya	-	Mwenyekiti
Deo Mwarabu	-	Makamu Mweyekiti
Revocatus Kasikila	-	Katibu
Agnes Namuhisa	-	Katibu Msaidizi
Chesco Sapula	-	Mhazini
Silvia Ishengoma	-	Mhazini Msaidizi

Kuanzia tarehe 1 Agosti 2007 mchakato wa uchaguzi wa viongozi wa halmashauri walei kijimbo na kitaifa ulianza. Kwa kigango chetu cha Makongo Juu, mchakato huu ulihitimishwa tarehe 17 Septemba 2007 kwa uchaguzi wa Kamati Tendaji ukisimamiwa na Paulo Sangu, katibu wa halmashauri ya walei jimbo. Katika uchaguzi huo, Kamati Tendaji chini ya uongozi wa Dk. Mary Mboya ilishiriki katika kupiga kura lakini uongozi hairakia wa Kanisa ulielekeza wasipigiwe kura kwa sababu za kichungaji. Katika uchaguzi huo wafuatao walichaguliwa.

Dkt. Camilius Lekule	-	Mwenyekiti
Benedict Mwobhahe	-	Makamu Mwenyekiti
Stephen Billa	-	Katibu
Teresia Wandiba	-	Katibu Msaidizi
Edwin Nnunduma	-	Mhazini
Magreth Ngeleja	-	Mhazini Msaidizi

Mei 13, 2007, uongozi hairakia wa Kigango uliwasimamisha uongozi Mwenyekiti na Mhazini wa Halmashauri ya Walei Kigango, kwa sababu za kiuchungaji, kufuatia Kigango cha Makongo Juu kutamkwa kuwa Parokia, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Katoliki la Dar es Salaam, Julai 15, 2007 alitengua Kamati Tendaji wa Kigango chini ya uwenyekiti wa Dk. Camilius Lekule na kuteua Kamati Tendaji ya mpito kama ifuatavyo;

Prof. Athanas Kauzeni	-	Mwenyekiti
Revocatus Kasikila	-	Makamu Mwenyekiti
Simon Billa	-	Katibu
Theresia Wandiba	-	Katibu Msaidizi
Joseph Lutege	-	Mhazini
Deo Mwarabu	-	Mjumbe
Menedora Liwa	-	Mjumbe

Uteuzi huu ulifanywa ili kuipa fursa Parokia mpya ya Makongo Juu kuanza ukurasa mpya na kusahau yote ya nyuma ya enzi za Kigango na kuganga mapya ya Parokia.

Mnamo tarehe 7 Julai 2007 ni siku ya kukumbukwa sana katika historia ya kigango cha Makongo Juu kwa sababu hiyo ndiyo siku ambayo matukio makuu manne ya kihistoria yalitokea kama ifuatavyo:

Mashemasi wawili Edwin Mwakigimba na Denis Wigira waliotumikia sehemu ya mwaka wao wa uchungaji katika Kigango cha Makongo Juu chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Padre Martin Dominic, Padre Mkazi, walipata Daraja ya Upadre.

Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam alikitamka Kigango cha Makongo Juu kuwa Parokia Mpya ya Makongo Juu.

Kutangazwa Parokia

Julai 7, 2007 ilikuwa ndio siku ya kuzaliwa Parokia ya Bikira Maria Mama wa Rozari Takatifu. Askofu Mkuu wa Dar es Salaam, Mwadhama Policarp Kardinali Pengo alitangaza kuwa Kigango cha Makongo Juu kimekuwa Parokia huku akimteua Mheshimiwa Padre Martin Dominic Rutayebesibwa, aliyekuwa Padre Mkazi wa Kigango cha Makongo Juu kwa kuwa Paroko wa Parokia ya Mlandizi na Mheshimiwa Padre Maximiliam Wambura, aliyekuwa Paroko Msaidizi wa Parokia ya Mburahati kuwa Paroko wa kwanza wa Parokia mpya ya Makongo Juu na pia alimteua Mheshimiwa Padre mpya Gaston Mkude aliyepewa daraja la Upadre siku hiyo kuwa Paroko Msaidizi wa Parokia mpya ya Makongo Juu.

Maparoko waliolichunga kundi la Mungu parokiani tangu kuanzishwa kwake ni Padre

Maxmillian Wambura (2007 – 2012)

Padre Gallen Mvungi (2012 – 2014)

Padre Joseph Massenge (2014 -)

Kufuatia Kigango cha Makongo Juu kutamkwa kuwa Parokia, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Dar es Salaam, Julai 15, 2007 alitengua Kamati Tendaji wa Kigango chini ya uenyekiti wa Dk. Camilius Lekule na kuteua Kamati Tendaji ya mpito kama ifuatavyo:

Prof. Athanas Kauzeni	-	Mwenyekiti
Revocatus Kasikila	-	Makamu Mwenyekiti
Simon Billa	-	Katibu
Theresia Wandiba	-	Katibu Msaidizi

Joseph Lutege	-	Mhazini
Deogratias Mwarabu	-	Mjumbe
Menedora Liwa	-	Mjumbe

Insert viongozi wa Kamati Tendaji tangu wa mwanzo hadi sasa

Ujenzi wa Kanisa

Mchakato wa kutafuta mchoro wa kanisa unaofaa ulianza na wachoraji wakashindanishwa. Mchakato wa ujenzi ulianza mwaka 2010. Hata hivyo, Jiwe la Msingi la kanisa jipya liliwekwa Septemba 22, 2012 na Mwadhama Kardinali na ujenzi ukaanza hatua kwa hatua.

Kamati ya Ujenzi iliundwa ambapo ilikuwa na wajumbe wafuatao:

Insert names

1

2

3

Hatua ya kwanza ya ujenzi ilihusisha uchimbaji wa visima viwili vya maji, kuhamisha barabara iliyokuwa inapita katikati ya kiwanja cha Kanisa na kutengeneza barabara mbadala inayozunguka kiwanja, kujenga uzio na kuchimba msingi mpaka kumwaga jamvi.

Hatua ya pili ilihusisha kujenga nguzo, beams na slab, kusanifu paa na kuezeka.

Hatua ya tatu inahusisha kuweka milango na madirisha, vigae vya sakafu, altare, mimbari za masomo na matangazo, kisima cha ubatizo na umaliziaji umaliziaji.

5. SAFU ZA UONGOZI WA KIGANGO (1978 – 2007)

5.1 Kipindi cha 1987 – 1990

1. T. Kasella – Mwenyekiti
2. S.G. Lyaruu – Mwenyekiti Msaidizi
3. D. Mizambwa – Katibu

5.2 Kipindi cha 1991 – 1994

1. C. Mwalongo – Mwenyekiti
2. D. Makene – Mwenyekiti Msaidizi
3. S. Billa – Katibu

4. M. Busanda – Mhazini

5.3 Kipindi cha 1995 – 1998

1. B. L. Mwobahe – Mwenyekiti
2. D. Meela – Mwenyekiti Msaidizi
3. T. J. Kasella – Katibu
4. J. M. Lutege

5.4 Kipindi cha 1998 – 2001

1. Benedict Mwobahe – Mwenyekiti
2. Timothy Kasella – Mwenyekiti Msaidizi
3. Mary Hokororo – Katibu
4. Leberatus Njau – Katibu Msaidizi
5. Joseph Lutege – Mhazini

5.5 Kipindi cha 2001 – 2004

1. Benedict Mwobhahe – Mwenyekiti
2. Rogat Kisanga/John Mongela – Mwenyekiti Msaidizi
3. Mary Hokororo/Simon Billa – Katibu
4. Simon Billa/Peter Mutungi – Katibu Msaidizi
5. Joseph Lutege

5.6 Kipindi cha 2004 – 22/10/2005[1]

1. Dk Raynold Mfungahema – Mwenyekiti
2. John Mongella – Mwenyekiti Msaidizi
3. Peter Mutungi – Katibu
4. Dk. L. Sayi – Katibu Msaidizi
5. Claud Makwinya – Mhazini

(SALA KWA MAMA BIKIRA MARIA WA ROZARI TAKATIFU SOMO KANISA LETU)

Tuombe:

"Ee Malkia wa Rozari Takatifu na somo wa Kanisa letu Salamu/ Kama ulivyobaini jinsi Maharusi wa Kana walivyotindikiwa divai/ na ukawaombea kwa Yesu, mzao mbarikiwa wa tumbo lako, wakapewa/nasi kwa matumaini hayo, tunakusihi mama wa Mungu/ uyabaini mahitaji ya Kanisa letu na utuombee kwa mwanao. Sisi Waamini wa Kanisa la Makongo/ katika ushirika wa wachungaji wetu, tunakuja mbele yako na kuomba pamoja nawe kwa unyenyekevu/ Mungu mwenyezi Baba wetu, tunakuja mbele yako na kuomba pamoja nawe kwa unyenyekevu/ Mungu mwenyezi Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo/ atupe Roho wa hekima na akili/ Roho wa ushauri na nguvu/ Roho wa elimu/ ibada na uchaji/ ili tuweze kuyafikia malengo ya Kiroho/ ya Kumjua

na Kumpenda Mungu tulivyojiwekea katika mpango wetu wa maendeleo ya maisha ya Kiroho

Roho wa Bwana afunue akili zetu na kutujalia moy wa ukarimu/ ili tutambue na kutekeleza kwa vitendo wajibu wetu wa kulitengeneza Kanisa "mahalia"/ liweze kustawi na hatimaye kutimiza utume wake kama Mwalimu wetu./ na mtoa neema za Mungu kwetu

Tunaomba hayo yote kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.